KONFERENSI YA KASKAZINI MASHARIKI MWA TANZANIA

# Semina kwa Kiongozi wa Mawasiliano

Semina hii imekusudiwa kumsaidia kiongozi wa mawasiliano kujua majukumu yake.

Na. Mch. Almodad Amos

Mkurugenzi wa Idara ya Mawasilino - NETC

# Idara ya Mawasiliano Kanisani

Karibu karne mbili zilizopita, jambo kubwa katika fikra za wanadamu ilikua ni kuisaka mali na pesa. Sasa hivi hali imebadilika, jambo lililo muhimu sana ni kupata habari.






TAKWIMU CHACHE ZA JINSI HABARI ZINAVYOKWENDA KWA KASI

- July 2015, wakazi wa ulimwengu Bilioni 7.3
- wanaotumia Internet Bilioni 3.17
- Wanaotumia mitandao ya kijamii 2.3
- 91% ya wafanya biashara wanatumia Mitandao 2 au zaidi
- Watumiaji wa internet kwa kawaida wanatumia mitandao 6
- Watu milioni 1 wanaotumia simu wanaongezeka kila siku
- Facebook na Whatsapp hurusha jumbe Bilioni 60

MAWASILIANO

- Ni njia inayotumiwa na viumbe hai ili Kubadilishana, Kufahamishana, Kujulishana au kutaarifiana mawazo, habari au hisia kutoka kwa mtu/kundi moja kwenda kwa mtu mwingine au kundi jingine.
- Kwa mujibu wa Biblia, siku hizi za mwisho kanisa linahusika sana na HABARI.... "***Tena habari njema ya ufalme itahubiriwa katika ulimwengu wote, kuwa ushuhuda kwa mataifa yote; hapo ndipo ule mwisho utakapokuja***. Mathayo 24:14"

KAULIMBIU YA IDARA – GC

- **Jenga madaraja ya matumaini:** Idara ya mawasiliano huhamasisha utumiaji wa programu thabiti ya uhusiano na mbinu zote za kisasa za mawasiliano, tekinolojia endelevu na vyombo vya habari katika kueneza injili... *Mwongozo wa kanisa (toleo 2010) uk 104*

IDARA YA MAWASILIANO

MAKUNDI MATATU ANAYOSHUGHULIKA NAYO KIONGOZI WA MAWASILIANO

| | |
|---|---|
| KANISA | NINI KINAENDELEA KANISANI KWAKO<br>**Wanaohudhuria kila siku, mara mojamoja, mara chache, kila siku, na hata waliorudi nyuma** |
| KONFERENSI | **KULIUNGANISHA KANISA LA ULIMWENGU**<br>**Machapisho, Picha, Taarifa, Habari** |
| JAMII JIRANI | **Watu wenye mtazamo chanya na hasi kwa Kanisa, wanaolifahamu sana na wasiojua lolote kulihusu kanisa. Hapa unatafuta namna ya kuwafanya watu walifahamu Kanisa na hatimaaye kuja kanisani**<br>**WAKRISTO, HESHIMA, UHAI WAKE, MSAADA, DUNIANI KOTE, KUKUA KWAKE, KANISA RAFIKI** |

**Sifa za kiongozi wa mawasiliano:**

- Kuliwakilisha kanisa vema
- Maamuzi ya busara
- Ushirikiano
- Kuandika taarifa/habari nzuri, za kweli, zenye mvuto
- Kuchanganyika na watu tofauti tofauti
- Nia ya kufanya kazi na kujifunza

**Kamati ya Mawasiliano**

- Katibu wa mawasiliano – M/KITI
- Mratibu wa sauti ya unabii
- Mtaalamu wa teknolojia ya Habati na mawasiliano (IT)
- Mwandishi wa habari
- Fundi mitambo wa kanisa

**VIFAA VYA MUHIMU**









- PROJECTOR
- SMART PHONE
- TABLETS
- LAPTOPS
- PRINTER
- CAMERA

YA MAWASILIANO - NEC

**NAMNA YA KUHABARISHA**




- Kuwe na kalenda za maukio za Konferensi makanisani ili zisaidie kujua matukio na program za konferensi makanisani.
- Zitasaidia kujipanga vema na kupunguza usumbufu wa viongozi kukosa matukio ya konfernsi kwa sababu wameshtukizwa au wamejisahau.

**Vibao vya matangazo (Notes Boards)**

- Ni njia rahisi ya kuwafikia washiriki hasa siku ya sabato
- Weka picha, matangazo, matukio yanayokaribia & Vipeperushi
- Usibandike mambo muhimu kaitka ukuta... weka katika mbao za matangazo

**Tengeneza Vipeperushi**

- Wapatie wageni
- Litambulishe kanisa lako
- Matukio yanayokaribia
- Vipindi  mbalimbali vya mafunzo ya Biblia
- Weka salam kutoka kwa mchungaji n.k.

**Tengeneza Vibao Elekezi**




- Viwekwe mahali panapoonekana
- View vibao vizuri sana
- Tangu sasa vitakuwa vikitengenezwa Union na kusambazwa Tanzania nzima

**Fanya Mahusiano mazuri na wahariri**

- Peleka habari katika Radio
- Peleka habari pia katika Runinga
- Na hata kwa waandishi wa magazeti
- Litangaze kanisa kila linapofanya jambo jema, ili umma utambue uwepo wa kanisa.

**Machapisho, Makala & Gazeti**




- Habari, Makala, Gazeti
- Uinjilisti kanisani
- Njia mpya za kufanya uinjilisti
- Huduma kwa jamii
- Maamuzi ya baraza juu ya mambo muhimu
- Shughuli mbalimbali zinazondelea kanisani k.v. Ushirika, mahudhurio
- Fedha za kanisa, kiasi kinachopatikana na kilichotumika
- Tuzo flani kanisani
- Mwitikio wa kanisa kwa mambo ya kijamii
- Kifo cha kiongozi au mshiriki
- Mambo yafurahishayo & yasiyo ya kawaida ktk huduma binafsi afanyazo mtu
- Nitumie habari ili watu waliombali na wewe wabarikiwe kwa program yako: tuma kwa: **modaofpeace@gmail.com**

IDARA YA MAWASILIANO - NETC

- **JINSI YA KUANDIKA HABARI**
    - Kichwa cha habari kiwe kizuri, chenye kuvutia, kifupi
    - Utangulizi uwe na ubunifu (nani, nini, lini, wapi)
    - Eleza umuhimu wa habari yako kwa ufupi (kwa nini msomaji aisome?)
    - Weka nukuu kutoka kwa kiongozi
    - Huduma iliyofanyika au tukio lilivyofanyika (lilifanyika namna gani)
    - Nukuu maneno ya waliohusika/waliokuwepo
    - Ita watu kujifunza/kutenda kama walivyojifunza katika habari yako

**Tembelea tovuti mbalimbali za kanisa ili upate habari**




- http://www.sdanet.org/ hapa utakuta anuani za tovuti mbalimbali zenye mambo yanayohusiana na kanisa
- https://www.adventist.org/ hata ni tovuti rasmi ya Kanisa la Waadventista Wasabato
- 

**Fungua tovuti kwa ajili ya kanisa lako bila kulipia**

- Tembelea www.netadventist.org

# Mitandao ya Kijamii na Uinjilisti

- Watu watatu kati ya watu wanne wanatumia mitandao ya kijamii
- Mitandao ya kijamii imechukua sehemu kubwa sana ktk matumizi ya mtandao kuliko barua pepe

**MITANDAO YA KIJAMII NI NINI?**

Ni njia ya kuchangia mawazo, fikra, habari, maarifa na kuanzisha/kuendeleza urafiki kwa kutumia njia ya mtandao. Inaweza ikawa kwa ujumbe mfupi wa maandishi, sauti, video au picha za mnato.

Ni njia ya mtandao inayomwezesha mtu kushiriki na kuchangia habari, picha, au video pale zinapowekwa/mtu anapojisikia huru kuziweka hadharani;

**TAKWIMU CHACHE ZA MITANDAO YA KIJAMII**

**FACEBOOK**

- Wanaotumia FACEBOOK ni watu milioni 500, Video bilioni 8 zinatazamwa kila siku
- Asiliamia 78% ya watumiaji wa internet wanatazama video za mtandaoni kila siku
- Watu wanatafuta vitu kwa kutumia Google mara bilioni kwa wiki 100
- Huu ni uwiano wa mara 40,000 kwa kila sekunde, zaidi ya nusu ya hao watafutao hutumia simu za mkononi.
- Watumiaji wa Facebook wanaendelea kuongezeka 500,000 kila siku karibu watu; 6 kwa kila sekunnde
- Mtu mmoja anawastani marafiki 338
- Nusu ya watu wasiotumia FACEBOOK wanaishi na watumiaji wa FACEBOOK kwa hiyo habari zinawafikia
- Asiliamia ya marafiki zako, 24% huangalia picha unazoweka FACEBOOK

**YOUTUBE**

- Video za masaa 300 zinawekwa mtandaoni kwa kila dakika
- Masaa bilioni 3.25 yabatumika kilamwezi, kuangalia video
- Zaidi ya nusu ya watumiaji wa mitandao hii wanatumia simu zao

**WHATSAPP**

- 

**MAMBO MUHIMU YA KUFAHAMU**

- **Chanzo cha habari**: Unda makundi ya whatsapp, facebook, uwepo twitter, instagram, n.k. watu sasa hivi wanaiamini sana mitandao ya kijamii kuliko wanavyoamini vifaa vya kutafutia habari mtandaoni ("search engines"). Sasabu ni kwamba wanamfahamu mtoa habari na wanaweza kuwasiliana naye kama wanahitaji au wanalo swali.
- **Kuhimiza matukio/shughuli muhimu**: mwitikio wa utekelezaji wa tukio au shughuli huwa mzuri tunapotumia mitandao ya kijamii, kwani marafiki huwashawishi marafiki wenzao kutekeleza jambo flani.
- **Hukupatia marafiki**: wapya na wale wa zamani. Watu ambao hukuwa na ukaribu nao, unaweza ukajenga nao urafiki kwa njia ya mitandao ya kijamii
- **Inakusaidia kuwafahamu watu wako vizuri**: jambo kubwa si nani kuonekana jinsi ulivyo sahihi ila jambo kubwa ni kutoa mawazo yako, hisia zako na kuonyesha picha ya ubinadamu wako.

IDARA YA MAWASILIANO - NETC

- **Kuna ushawishi mkubwa sana katika hii mitandao ya kijamii**: kwa sababu ya shinikizo rika, shinikizo jamii au ushawishi wa msemaji ikiwa anao mvuto kwa wana kundi.

## Faida za kuitutmia mitandao ya kijamii

1. Kuvumiliana. Mitandao ya kijamii ni mizuri sana kwa kuficha tofaui zetu. Huoni mwonekano, rangi ya mtu au umbo lake. Mtu anashughulika na umuhimu au uzito wa habari.
2. Urafiki. Mitandao ni kama muunganiko wa mafundo. Unarafiki ambaye anamjua rafiki mwingine awezaye kukuunganisha na kundi flani la watu.
3. Kuendana na mazingira. Habari zinazotumwa kwa mitandao ya kijamii zaweza kwenda kwa mazingira yoyote na kumfikia yeyote bila kujali mitazamo yake mwitikio wake.
4. Kuunganika na jamii. Makundi hiuundwa ili kuwe na kujumuika pamoja kama wanajamii moja.
5. Habari huru. Katika miaka iliyopita, waandshi wa habari walichambua nini kizungumziwe katika runinga au katika redio. Sasa hivi kila mtu anaouhuru wa kusema anavojisikia na kutoa habari yake nila kizuizi (alimradi tu hapingani na sharia ya nchi).
6. Habari inaweza kuenea ulimwengu mzima bila kujali mipaka ya kimaeneo
7. Kila mmoja anaweza kushirki vizuri kabisa katika hoja au habari inayotolewa
8. Kanuni mpya katika ulimwengu wa habari ni kwamba: usipoileta, mtu mwingine ataileta kwa jinsi usivyotaka

Uinjilisti wa mitandao ya kijamii ni njia mpya ya uinjilisti ambayo iko mstari wa mbele katika uinjilisti, imejengeka katika msingi wa njia ya Kristo ya kuchangamana na watu mahali walipo, kutambua shida zao, kuwapatia mahitaji yao, na kuwaalika kumfuata Yesu.

Njia ya Yesu ya kusambaza injili ilijikita katika ufuasi (kuwafanya watu kuwa wanafunzi). Tunatamani kutumia njia hii katika nyakat zote za uinjilisti wa mtandao. Wamishonari wa mtandaoni wanatakiwa kuwaona watu wao (ambao ni anuani walizonazo) kama fursa ya maana kabisa ya kuwafanya kuwa wanafunzi na wafuasi wa Yesu, na kila mchungaji aliye mtandaoni anapaswa kumchukulia kila mwanamtandao kama mwanafunzi wa yesu.

Wanafunzi mtandaoni, ni sawa tu na wanafunzi tunaokutananao uso kwa uso. Ikiwa tunafuata njia ya Kristo ya kuwafikia watu, tunaweza kuona kwamba muda aliutumia pamoja na watu akiwafanyia yaliyo bora kabisa. Alijihusisha na kutambua shida walizokuwa nazo, na ilipowezekana, alitatua matatizo yao. Mambo yote haya yaliwafanya watu aliokuwa nao karibu wampende, na baada tu ya hili kutokea angaliwaalika kumfuata. Kwa kutumia njii hii, hapa yapo mambo kadhaa ambayo ni njia ya uinjilisti wa mtandao wa kuwafanya watu kuwa wanafunzi:

- PATIKANA MTANDAONI: mitandao ya kijamii, Blogs, chatrooms, na mitandao ya mambo mbalimbali.
- TUMA VITU MTANDAONI: tuma vitu vinavyogusa mahitaji ya watu na waalike watu kuona vitu mbalimbali vinavyohusu maisha yao ya kila siku kupitia Videos na Makala mbalimbali

IDARA YA MAWASILIANO - NETC

- ZUNGUMZA: zungumza (chat) na marafiki zako wanaopatikana mtandaoni ili uelewe shida zao, na wajibu kwa ujumbe mahususi wa matumaini kutoka katika Biblia, na huenda kwa kutoa ushuhuda wako kwao.
- WATAFUTE na uonane nao uso kwa uso na uwakuze Imani yao katika kumtegemea Yesu.
- WAALIKE kumfuata Yesu katika safari ya maisha ya kiroho.

Makusudi yako, katika kila hatua, inatakiwa kumchukulia kima mtu mtandaoni kama mwanafunzi na mfuasi muhimu kabisa wa Yesu. Unatakiwa kuwa makini kabisa na jinsi wanavyoonesha mwiitkio wao kwa Yesu. Pia ni vizuri kuelewa kwamba huwezi ukatarajia kufuasa watu 500 mpaka 1000 kwa wakati mmoja, tena kwa mtu mmoja mmoja, bali unaweza kutumia muda wako vizuri kufuasa kundi la watu wachache na kujenga nao uhusiano mzuri.

Mahusiano haya binafsi yataunda umoja wa muhimu kabisa katika kujenga jamii ambayo itawaleta watu tena na tena katika uinjilisti wako wa mtandao wa kijamii.

Mtandao huu unakwenda Zaidi ya mahusiano ya kidijitali. Na hatimaye kila mwanafunzi atakuwa mshiriki halisi katika kanisa mahalia mahali flani, mahali flani katika jamii yake. Hili ndilo lengo kuu la uinjilisti wa mtandao: uhusiano wa kidijitali na wanafunzi halisi, na kuwaongoza kuwa washiriki halisi katika makanisa halisia mahali flani.

**TUFANYE NINI KAMA KANISA**

- Tuunde makundi ya mitandao ya kijamii FACEBOOK, TWITTER, WHATSAPP, INSTAGRAM, YOUTUBE, n.k.
- Kiongozi wa mawasiliano, mratibu wa wasikivu, mzee wa kanisa, n.k. wawe katika makundi ya mitandao ya kijamii.
- Tambua maisha ya jamii wako
- Shiriki nao habari/matangazo ya kanisa
- Jadilini mambo ambayo yanawatatiza watu
- Andika ombi na uliweke kwenye kundi lililoundwa kila mwanzo wa juma.
- Tumia mitandao ya kijamii kuwasiliana na wanakamati wenzako
- Shauri na tia moyo kwa kutuma jumbe fupi za maandishi
- Onyesha kukubaliana na vitu vizuri kama mtu akiweka jambo jema.
- Tumia facebook, twitter na whatsapp kuunda makundi ya kuwasiliana na wenzako
- Wafuase watu kwa Yesu. Mafundisho ya Biblia, Imani za msingi.
- Imarisha urafiki wako na waumini wako.


IDARA YA MAWASILIANO - NETC

## MFUMO WA USIMAMIZI WA MAKANISA YA WAADVENTISTA WA SABATO ULIMWENGUNI (ADVENTIST CHURCH MANAGEMENT SYSTEM)

- Ni mfumo unaotunza kumbukumbu za makanisa, washiriki, viongozi na wachungaji wa kanisa la Waadventista wa Sabato duniani
- Ni mfumo unaosaidia kufahamu ofisi na majukumu ya kanisa mahalia, konferensi, union, division na General Conference.
- Wazo lililetwa na Katibu mkuu wa GC Mchungaji G.T. Ng mwaka 2012
- "kanisa limekua na mfumo mzuri wa kutunza kumbukumbu za fedha kuliko washiriki." G. T. Ng na ndipo Akachaguliwa Ndugu Andrew Kuntaraf kusimamia zoezi hilo mwaka 2012.
- Baada ya hapo Mkutano wa wanateknolojia ya habari na mawasiliano ulifanyika tarehe 15 May 2013 ili kuweza kuuboresha mfumo huu kule Dubai.
- August 2013, GC Executive committee ikamchagua Sherri Ingram-Hudgins kuwa Director wa ACMS
- Septemba 2013 ACMS ikawaimeingia Tanzania.

## FAIDA ZA ACMS

1. Hurahisisha utunzaji wa kumbukumbu




2. Hurahisisha utunzaji wa kumbukumbu za kanisa (vikao,agenda,mali n.k)
3. Ni Njia ya Takwimu sahihi za wakati husika za washiriki
4. Huharakisha uhamaji wa mshiriki toka kanisa moja kwenda linguine
5. Husaidia ukuaji wa kiroho kwa washiriki
6. Hurahisisha kazi kwa mchungaji kujua washiriki wake
7. Ajira
8. Jicho la Kanisa

## MALENGO KWA MWAKA 2018

50% ya makarani wa kanisa wawe na elimu ya awali ya komputa
100% ya wachungaji wawe na Komputa
80% ya makanisa, washiriki na wachungaji wapya wawe wanaingia moja kwa moja kwenye ACMS
80% ya makanisa, washiriki na wachungaji wawe wamesajiliwa kwenye Mfumo
50% ya viongozi wa kanisa na wachungaji wawe na uwezo wa kutumia mfumo wa ACMS


## Radio na Television

Uongozi wa Radio na TV umeunganishwa na kuwa mmoja hivyo kupunguza matumizi ya raslimali watu.
Union ya Kusini imeanza kutoa sadaka ya vyombo vya habari kwa 8%
Mafundi na Warushaji wa Matangazo wamepata uzoefu wa kuwawezesha kuchagua njia bora za matangazo
Madeni yamelipwa kwa 70%




IDARA YA MAWASILIANO - NETF

## MPANGOKAZI WA IDARA YA MAWASILIANO KATIKA MUHTASARI












IDARA YA MAWASILIANO